

OFISI YA RAISI- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMSHAURI YA WILAYA YA ULANGA

SHULE YA SEKONDARI ISONGO,
S. L. P. 70,
MAHENGE / ULANGA
15/12/2020

Kwa mzazi / mleziwa

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE

Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na shule ya **SEKONDARI YA ISONGO** kidato cha kwanza kwa mwaka wa masomo 2021.

Aidha uongozi wa shule tunatumia fursa hii kukupongeza na kukukaribisha Isongo Sekondari.

Isongo Sekondari ni shule ya serikali ya kutwa kwa wasichana na wavulana, ipo umbali wa kilometa nne kutoka yalipo makao makuu ya wilaya ya Ulanga katika mji wa Mahenge.

Shule itafunguliwa rasmi kwa muhula wa kwanza tarehe **11/1/2021**.

Aidha utatakiwa kujibidisha katika masomo yako kwa muda wote utakaokuwepo hapa shuleni kama mwanafunzi na kusiwepo uzembe na uvivu wa kujifunza.

SARE ZA SHULE

▪ **WAVULANA:**

- ❖ **SURUALI:**Rangi ya kitambaa ni kijivu iliyoshonwa kwa kuzingatia maadili, isiwe ya kubana na lazima iwe na marinda mawili.
- ❖ **SHATI:** shati la kitambaa cheupe la mikono mifupi, lisilobana mwili na liwe refu la kuweza kuchomekea kwenye suruali.
- ❖ **VIATU:** Vyeusi vya ngozi vya kufunga na Kamba.
- ❖ **SOKSI:** Ndefu za rangi nyeupe.

▪ **WASICHANA:**

- ❖ **SKETI:** Kitambaa kizito cha rangi ya karoti, mashono yake ni ya rinda boksi, ndefu hadi chini ya magoti.
- ❖ **SHATI:**Nyeupe isiyobana mwili.Ndani ya shati msichana atavaa nguo nyingine nyeupe(shumizi)kwa lengo la kusitili mwili wako.

NB: Kwa wanafunzi wa kiislamu watakaohitaji kuvaa hijabu, watavaa hijabu za rangi nyeupe na ziwe kama kitambaa cha shati la shule na zisiwe na urembo wa aina yoyote ile.

- ❖ **VIATU:**Rangi nyeusi vya kufunga kwa kamba na view vya visigino vifupi.viatu vya wazi (open shoes),yeboyebo na bajaji haviruhusiwi.
- ❖ **SOKSI:**Rangi ni nyeupe zisiwe na alama wala maandishi ya aina yoyote ile.

- **SARE ZA MICHEZO NA NGUO ZA KAZI ZA NJE.**

Kwa wanafunzi wa kike na wakiume sare hizo ni T-shirt **dark blue** yenye shingo duara kwa ajili ya shughuli za kazi za nje za mikono,pia watatakiwa kuvaa ama sketi ya shule au suruali pamoja na hiyo T-shirt wakati wa kazi.

- ❖ Wakati wa michezo mwanafunzi atatakiwa kuwa na bukta ya bluu au track suit kwa wavulana pamoja na T-shirt zao bluu. kwa wasichana ni track suit ya bluu pamoja na T-shirt zao bluu.
- ❖ Pia wakati wa michezo mwanafunzi utatakiwa kuwa na viatu vya **raba**.
NB:T-shirt hazitakiwi kuwa na maandishi ya aina yeyote ile.


- **VIFAA VYA DARASANI:**

- ❖ Madaftari 11(kumi na moja)counter book quire 2au 3 kwa ajili ya masomo kumi na moja utakayokuwa unajifunza hapa shuleni.
- ❖ Mkebe wa hisabati (mathematica set).
- ❖ Peni iwe bluu au nyeusi.
- ❖ Rula,penseli,kifutio n.k

NB:Kutokanaa na uhaba wa vitabu uliopo hapa shuleni kwa masomo ya sanaa na lugha unashauriwa kununua vitabu kwa ajili yako ili kuongeza ufanisi katika kujisomea kwako .masomo hayo ni Historia, Jiografia, Uraia, Kiingereza, na Kiswahili.

Utakapofika shuleni utapewa na kuelekezwa sheria za shule ambazo katika kipindi chote utakapofika shuleni utatakiwa kuzifuata,kuzitii na kuziheshimu,kinyume na hapo utapewa adhabu kali ikiwa pamoja na kufukuzwa shule.

Nakukaribisha sana **ISONGO SEKONDARI** shule yenye mandhari nzuri ya kujisomea.

Sc mfungahema 
SECILIANO CRISPIN MFUNGAHEMA
MKUU WA SHULE

MKUU WA SHULE
ISONGO SEKONDARI
S.L.P. 70
L. M. 1111111111111111